RISE
RESEARCH ON IMPROVING SYSTEMS OF EDUCATION

INSIGHTS

Motisha, Changamoto, na Tabia za Watoa Huduma Mstari wa Mbele wa Elimu Tanzania

Jacobus Cilliers na Shardul Oza
Anthony Mwambanga (tafsiri)
Timu ya Utafiti ya RISE Nchini Tanzania

Dondoo Muhimu

- Ma-AEK wanawajibika kwa shughuli anuwai wanapotembelea shule, lakini kuna tofauti kubwa kati ya wilaya na wilaya kwa kile wanachofanya. Matokeo haya yanaonyesha kuwa serikali na wadau wengine wa elimu wana kazi kubwa ya kufanya katika kulinganisha shughuli wanazofanya ma-AEK na kulenga zaidi zile ambazo zitaboresha ubora wa shule.
- Mara nyingi ma-AEK hukosa rasilimali wanazohitaji kwa ajili ya kutembelea shule. Pamoja na kuwa karibu ma-AEK wote nchini Tanzania wamepokea pikipiki za kutembelea shule, wengi wao bado hawana bajeti ya kutosha kwa ajili ya mafuta na matengenezo.
- Pamoja na kuwa ma-AEK wanaonesha kuridhika na kazi zao kwa ujumla. Lakini, hawaridhishwi na mishahara yao pamoja na na fursa za upandaji vyeo/madaraja
- Ma-AEK wanakumbusha kuwa ni nadra sana kwa wao kuzawadiwa, ingawa wanaamini kwamba wasimamizi wao wanajua kuwa wanafanya kazi vizuri.
- Ingawa ma-AEK wanaripoti kuwa na kiwango cha juu cha mamlaka na maamuzi binafsi, kazi zao huwa ngumu zaidi kwa sababu ya ukweli kwamba watu tofauti wanahitaji au wanatarajia vitu tofauti kutoka kwao.

Utangulizi

Je! Serikali na watendaji/wadau wengine wa elimu wanawezaje kuboresha utoaji wa huduma ya elimu? Nchini Tanzania, Maafisa wa sekta ya umma wanaojulikana kama Maafisa Elimu Kata (ma-AEK) ndio wenye jukumu kuu katika kufuatilia ubora wa elimu ya msingi. Maafisa Elimu Kata ni maafisa wa serikali za mitaa ambao huwasiliana mara kwa mara na shule na wana majukumu anuwai ambayo ni pamoja na kufuatilia uboreshaji wa shule, kusaidia walimu, na kukusanya taarifa za ngazi ya shule. Katika miaka ya hivi karibuni, Serikali ya Tanzania na wahisani wamekuwa wakijaribu kuimarisha majukumu ya Afisa Elimu Kata kwa kuwapatia rasilimali, mafunzo, na majukumu makuu katika programu za kielimu. Kwa mfano, mfumo mpya wa Serikali wa Uthibiti Ubora wa Shue umeainisha majukumu muhimu ya Maafisa Elimu Kata katika kufuatilia mapendekezo yatokanayo na Ziara za Jumla za Shule (Uthibiti Ubora wa Shule). Miongoni mwa sababu za kuhamishia rasilimali na majukumu kwa ma-AEK ni imani kwamba maafisa hawa walio mstari wa mbele wana uhusiano, taarifa na uaminifu unaohitajika katika kuathiri mabadiliko chanya katika ngazi ya shule.

Katika andiko hili, tunatumia taarifa kutoka katika utafiti wa kitaifa uliofanywa mwaka 2019 katika kutoa mwanga juu ya kile ambacho ma-AEK hufanya, ufahamu wao juu ya majukumu yao wenyewe, na vikwazo wanavyokabiliana navyo katika kutekeleza wa majukumu yao. Tuliwahoji ma-AEK 397 wanaohusika na shule za msingi katika wilaya 23 na mikoa sita ya Tanzania kama sehemu ya utafiti wa kimsingi uliofanywa kati ya Februari na Mei 2019. Andiko hili linachangia ukuaji wa fasihi juu ya shughuli, mitizamo binafsi, na kuwapatia motisha maafisa wa sekta ya umma ambao ndio wasimamizi wa mwisho katika utoaji wa huduma. Kwa mfano, Aiyar na Bhattacharya (2016) hutumia ‘time-use diaries’, mahojiano ya kina, na taarifa za vipimo mbalimbali kuelewa maoni, mitazamo, na shughuli za maafisa wa sekta ya elimu wa ngazi ya chini ya wilaya, ambao huitwa ‘block education officers’, nchini India.[1]

[1] Aiyar, Yamini, and Shrayana Bhattacharya. “The post office paradox.” Economic Political Weekly 51.11 (2016).

Usuli

Nchini Tanzania, wizara mbili tofauti zinahusika na elimu ya msingi: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inaongoza juhudi za upangaji sera wakati Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (pia inajulikana kama PO-RALG au TAMISEMI) hii inasimamia shughuli za kila siku za shule na utekelezaji wa sera. TAMISEMI inaajiri maafisa katika ngazi ya mkoa, wilaya, na kata ambao wanahusika na utoaji wa elimu. Kata ni ngazi za chini za utawala wa kiwilaya ambazo hujumuisha vijiji/mitaa kadhaa. Afisa Elimu wa Kata anaripoti moja kwa moja kwa Afisa Elimu wa Wilaya ambaye naye huripoti kwa Afisa Elimu wa Mkoa. Kila mmoja wa maafisa hawa wa elimu pia huingiliana mara kwa mara na mtendaji mkubwa katika vitengo vyao vya utawala ambaye pia ni mwajiriwa wa TAMISEMI. Katika ngazi ya kata, afisa huyu ndio Afisa Mtendaji wa Kata, anayesimamia shughuli zote za wizara/kielimu ndani ya kata.

Katika andiko hili, tunachunguza ikiwa tabia na maoni binafsi yaliyoripotiwa na ma-AEK hutofautina kupitia uelewa wao juu ya programu kubwa inayofadhiliwa na wafadhili iitwayo EQUIP-T. Programu ya Kuboresha Ubora wa Elimu (EQUIP-T) ilikuwa mradi wa GBP milioni 84.5 uliofadhiliwa na Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (DFID) ambayo ilifanya kazi katika mikoa tisa ya Tanzania kati ya mwaka 2014 na 2020. Lengo kuu la mradi huo, ambao ulilenga wanafunzi milioni 3.2 na walimu 55,000 katika shule 5196, ilikuwa kuboresha matokeo ya ujifunzaji wa elimu ya msingi nchini Tanzania. Programu hiyo iliangazia na kuzingatia maeneo matano:

1. Kuboresha upatikanaji wa elimu bora
2. Kuimarisha uongozi na usimamizi wa shule
3. Kuimarisha mipango na usimamizi wa wilaya
4. Ushirikishwaji wenye nguvu wa jamii na kudai uwajibikaji katika elimu
5. Kuboreshwa kwa ujifunzaji na upatikanaji wa taarifa

Mradi uliwasaidia Maafisa Elimu wa Kata kwa kuwapatia misaada na pikipiki, rasilimali ambazo zingewawezesha kufanya ziara zaidi za shule. Zaidi ya kupokea rasilimali za ziada, ma-AEK katika maeneo ya mradi wa EQUIP-T walishiriki katika kikao Endelevu cha kila mwezi cha Maendeleo ya Kitaaluma (CPD) na mafunzo juu ya majukumu yao. Programu nyingine kubwa inayofadhiliwa nchini Tanzania iitwayo TUSOME pia imejikita katika kuboresha ujifunzaji wa madarasa ya awali. Lakini, kwa kuwa sampuli yetu haijumuishi mkoa wowote ambao mradi wa TUSOME unafanyika, hatukuweza kuchunguza matokeo ya mradi huo.

Je! ma-AEK hufanya nini?

Kielelezo namba 1 kinaonesha sehemu ya muda ambao ma-AEK hutumia katika shughuli mbalimbali rasmi. Ma-AEK hutumia muda wao mwingi (asilimia 55) kutembelea shule, ukweli ambao unathibitisha jukumu lao muhimu kama wachunguzi/wafuatiliaji wa mbele. Ma-AEK pia hutumia sehemu kubwa ya muda wao kuandika ripoti (asilimia 17), kuhudhuria mikutano (asilimia 17), na kushiriki katika mafunzo (asilimia 9).

Kielelezo cha 2 kinaonesha kwamba kuna tofauti kubwa kiwilaya ya shughuli azofanya AEK wakati wa ziara za shule. Sehemu kubwa ya ma-AEK karibu wilaya zote wameelezea kukagua nyaraka za shule wakati wa ziara zao. Takribani asilimia 75 ya ma-AEK katika sampuli yetu wameelezea kwamba wanakagua nyaraka za shule wakati wa ziara. Lakini, tunaona tofauti kubwa zaidi ya kiwango cha wilaya katika shughuli zingine kama vile kutathmini wanafunzi. Kwa mfano, wakati ni asilimia 7 tu ya

Kielelezo cha 1. Je! Ma-AEK hutumiaje muda wao?



Kumbuka: Sampuli hii ya ya ma-AEK wote (n=397)

ma-AEK katika wilaya ya Rufiji waliripoti kwamba wanafanya tathmini ya wanafunzi, karibu asilimia 77 ya ma-AEK katika wilaya ya Kakonko hufanya hivyo. Utofauti mkubwa kati ya wilaya unaonyesha kwamba usimamizi wa ngazi ya wilaya au mambo mengine ya ndani huathiri tabia ya ma-AEK. Serikali ya Tanzania ingeweza kufanya kazi kuhakikisha kuwa ma-AEK wanajikita zaidi katika kuzingatia shughuli ambazo zinahusiana sana na kuboresha matokeo ya ujifunzaji kama vile kutathmini wanafunzi, kuchunguza ufundishaji, na kuwapati walimu mrejesho.

TTulichunguza pia ikiwa kuna tofauti katika shughuli wanazofanya ma-AEK katika wilaya ambazo kuna Programu kubwa zinazofadhiliwa na wahisani, Programu ya Kuboresha Ubora wa Elimu - Tanzania (EQUIP-T), ilifanya kazi kati ya mwaka 2014 na 2020. Hatuoni tofauti kubwa katika shughuli ambazo ma-AEK hushiriki kati ya wilaya ambazo mradi wa EQUIP-T unafanya kazi na wilaya ambapo hakuna mradi huo.

Kielelezo cha 2: Je! ma-AEK hufanya nini wakati wa ziara za shule (kwa wilaya)?

Kumbuka: Kila nukta inawakilisha sehemu ya wastani wa AEK katika wilaya ambayo waliripoti kushiriki katika shughuli hiyo wakati wa ziara ya shule, n = wilaya 23.

Rasilimali

Utafiti unathibitisha kuwa ma-AEK wanakabiliwa na vikwazo vya kirasilimali. Wakati karibu ma-AEK wote katika sampuli yetu hutumia pikipiki za serikali kutembelea shule zao (asilimia 94), Ni (asilimia 46) ambao ni chini ya nusu ndio wana bajeti ya matengenezo wakati (asilimia 24) wana bajeti ya mafuta. Hii inamaanisha kuwa ma-AEK wengi hutumia pesa zao za mfukoni kutekeleza majukumu yao kikazi. AEK mmoja kati ya ma-AEK kumi ana nafasi ya kutumia kompyuta. Sehemu ya juu zaidi ya ma-AEK wana nafasi ya kutumia vishikwambi (asilimia 42) lakini hii inasababishwa zaidi na uwepo wa mpango wa EQUIP-T, ambao ulisambaza vishikwambi kwa ma-AEK kama sehemu ya shughuli zake.

Kielelezo cha 3: Je! Ni rasilimali zipi ambazo ma-AEK wanazo?



Kumbuka: Sampuli hii ni ya ma-AEK wote (n = 397). Ukitembea kutoka kushoto kwenda kulia, baa zinaonyesha sehemu ya ma-AEK ambao (i) wana bajeti ya matengenezo, (ii) bajeti ya mafuta, (iii) wanamiliki kompyuta, na (iv) wanamiliki vishikwambi.

Tuligundua kwamba rasilimali ambazo ma-AEK wanazo hutofautiana sana kwa kulingana na uwepo wa mpango wa EQUIP-T katika eneo husika. Kielelezo cha 4 kinaonyesha kuwa sehemu kubwa zaidi ya ma-AEK katika wilaya za EQUIP-T wanaripoti kuwa na bajeti za mafuta na matengenezo zinazojitosheleza kumaliza majukumu yao yote ikilinganishwa na wenzao walioko katika wilaya zisizo na EQUIP-T. Karibu sita katika kumi (asilimia 59) ya ma-AEK katika wilaya za EQUIP-T wanakubali au wanakubaliana sana na kauli isemayo “Nina rasilimali za kutosha kufanya kazi yangu vizuri” ikilinganishwa na 4 kati ya 10 (asilimia 37) ya ma-AEK katika wilaya zisizo na mradi wa EQUIP-T.

Kielelezo cha 4: Upatikanaji wa Rasilimali kwa maeneo EQUIP-T na yasiyo na mradi



(a) Mafuta *(b) Matengenezo* *(c) Kwa ujumla*

Kumbuka: Tofauti ya wastani kati ya maeneo ya EQUIP-T (rangi ya machungwa) na maeneo yasiyo na EQUIP-T (rangi ya buluu). Paneli A, B na C zinaonesha sehemu ambazo zinaripiti kuwa na: (i) kuwa na bajeti ya kutosha ya mafuta, (ii) kuwa na bajeti ya kutosha ya matengenezo, na (iii)kukubali au kukubali sana kauli isemayo “ Nina rasilimali za kutosha kufanya kazi yangu kwa ufasaha”

Matokeo yetu yanaonyesha kuwa rasilimali za ziada zilizotolewa na EQUIP-T zilisababisha kuongezeka kwa ziara zaidi za ma-AEK shuleni. Kielelezo cha 5 kinaonyesha kuwa ma-AEK katika maeneo ya mradi wa EQUIP-T walitembelea shule 4 zaidi kwa wastani katika kipindi cha wiki mbili ikilinganishwa na wenzao katika maeneo yasiyo na mradi wa EQUIP-T, ambayo ni tofauti ya asilimia 11. Ikiwa tofauti hii itaendelea kwa kipindi cha mwaka, ma-AEK katika maeneo ya EQUIP-T watatembelea takriban ziara 8 zaidi za shule kuliko wenzao wasio katika maeneo ya mradi wa EQUIP-T. Ma-AEK katika maeneo ya mradi wa EQUIP-T hawatumii sehemu kubwa zaidi ya muda wao kutembelea shule (Kielelezo cha 5b), matokeo ambayo yanaonyesha kwamba labda wanaweza kutumia muda wao kwa ufanisi zaidi (kwa kufanya ziara zaidi za shule ndani ya muda huo huo).

Kielelezo cha 5: Ziara za shule za ma-AEK kwa maeneo ya EQUIP-T vs. maeneo yasiyo na -EQUIP-T



(a) Shule zilizotembelewa *(b) Muda uliotumika*

Kumbuka: Tofauti ya wastani kati ya maeneo ya EQUIP-T (rangi ya machngwa) na maeneo yasiyo na EQUIP-T (rangi ya buluu). Paneli A inaonesha idadi ya shule zilizoripotiwa kutembelea na ma-AEK katika kipindi cha wiki mbili zilizopita (n = 397). Paneli B inaonesha sehemu ya wakati kwa ujumla uliotumiwa na ma-AEK kutembelea shule (n = 394).

Kuridhika na kazi/Motisha

Kielelezo cha 6 kinaonyesha kuwa ma-AEK wameridhika kabisa na vitu vingi katika majukumu yao ikijumuisha na meneo yao ya kazi zao, msaada wanaopata kutoka idarani, na uhakika wa kazi ambao nafasi hiyo inawapatia. Lakini, ni ma-AEK wachache wanaoridhika na fursa za kupanda madaraja/vyeo au mishahara yao. Karibu robo tatu ya ma-AEK (asilimia 73) wameridhika kiasi au wameridhika sana na fursa za kupanda daraja/vyeo na zaidi ya nusu ya ma-AEK (asilimia 57) wameridhika kiasi au wameridhika sana na mshahara wao. Ni mmoja tu kati ya ma-AEK kumi (asilimia 9.3) ndio ameridhika sana na mshahara wake.

Suala la kuwa chini ya kiwango cha kidunia katika kuridhika na fursa za upandaji/vyeo inaweza kusababishwa na ufinyu au ukosefu wa kukua kicheo ndani ya nafasi ya u-AEK au zaidi ya kiwango cha Afisa Elimu wa Wilaya. Zaidi ya nusu ya ma-AEK (asilimia 57) wanapendekeza kuwa wangependa kupata nafasi ya AEW ndani ya miaka 5 ikiwa kila kitu kinakwenda kulingana na mipango na wachache wameonesha kuwa na matarajio zaidi ya kiwango cha AEW. Ili kuboresha uridhikaji wa ma-AEK kazini, serikali inaweza kuzingatia kuongeza mishahara na kuwatengeneza fursa zaidi za kuendeleza taaluma zao.

Kielelezo cha 6: Je! Unaridhika kwa kiasi gani na mambo yafuatayo katika kazi yako?



Kumbuka: Sampuli hii ni ya ma-AEK wote. Urefu wa baa za buluu na kijivu inaonyesha kiwango cha kuridhika sana na kuridhika. Ukitembea kutoka kushoto kwenda kulia ni vitu ndani ya kazi kama: 1) Msaada kutoka Idara Wilayani; 2) Fursa ya kuleta mabadiliko chanya; 3) Eneo la Kazi la Sasa; 4)Fursa za Kupanda Daraja/Cheo; 5) Mshahara wa Sasa; 6) Kuwa na kazi thabiti na kipato

Tuliwauliza ma-AEK pia ikiwa wanakubali au hawakubaliani na kauli mbalimbali kuhusiana na na majukumu yao. Matokeo yanaonyesha kuwa sehemu kubwa ya ma-AEK wanaamini wana mamlaka na uwezo juu ya majukumu yao. Kwa mfano, asilimia 93 wanakubali au wanakubaliana sana na kauli isemayo “Mimi na wafanyakazi wenzangu tuna mamlaka ya kutosha kufanikisha kazi zetu kwa mafanikio” na asilimia 95 wanakubali au wanakubaliana sana na kauli isemayo “Mimi na wafanyakazi wenzangu tumepewa maamuzi/uhuru wa kutosha kukamilisha majukumu yetu.” Tathmini binafsi ya ma-AEK wenyewe kama wahusika huru ndani ya uongozi wa kirasimu hutofautiana na ile ya maafisa sawa na wao katika mazingira mengine ya nchi tofauti zinazoendelea. Katika kitabu chao Aiyar na Bhattacharya cha (2016) waligundua kwamba maafisa hawa ‘kimsingi hujiona kama kiunganishi muhimu katika gia za meno’. Ingawa ma-AEK wengi wanaridhika na uhuru wao na nguvu ya kufanya maamuzi, wachache wana maoni mazuri juu ya zawadi

wanazopokea. Ni ma-AEK sita tu kati ya kumi wanakubali au wanakubaliana sana na kauli isemayo “Ninazawadiwa na meneja/msimamizi wangu pale ninapofanya vizuri”. Hii inaonyesha kwamba kuna nafasi kwa serikali kujenga mfumo bora wa tuzo/zawadi kwa ma-AEK wanaofanya vizuri.

Kielelezo cha 7: Ni kwa kiasi gani unakubaliana na kauli zifuatazo?



Kumbuka: Angalia Kielelezo cha 7. Ukitembea kutoka kushoto kwenda kulia, kauli ni: 1) Mimi na wenzangu kazini tuna mamlaka ya kutosha kufanya kazi zetu kwa mafanikio; 2) Ninapata ugumu kumaliza majukumu yangu yote kwa sababu watu tofauti wanatarajia vitu tofauti kutoka kwangu; 3)Mimi na wafanyakazi wenzangu tumepewa mamlaka ya kutosha kufanikisha kazi zetu; 4) Ninatuzwa/kuzawadiwa na msimamizi wangu ninapofanya vizuri.; 5) Pale mimi na wenzangu tunapofika kazini kila siku huwa tuna ufahamu wa kutosha juu ya majukumu na matarajio yetu na kile ambacho AEW anatarajia kutoka kwetu; 6) Msimamizi wangu anajua pale ninapofanya vizuri na pale ambapo sifanyi vizuri.

Karibia robo tatu ya ma-AEK (asilimia 74) wanakubali au wanakubaliana sana na kauli isemayo “Ninapata ugumu kumaliza majukumu yangu kwa sababu watu tofauti wanatarajia vitu tofauti kutoka kwangu.” Matokeo haya yanaonesha kwamba ma-AEK wana watendaji wengi juu yao ambao wanahitaji vitu vingi kutoka kwao. Ma-AEK wapo chini ya Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, wizara inayosimamia shughuli za kielimu za kila siku. Hata hivyo, wanaweza kulazimika kuitikia wito kutoka kwa maafisa wengine wa serikali za mitaa kama vile Madiwani wa Kata au mahitaji mengine kutoka kwa wizara inayosimamia utengenezaji wa sera za sekta ya elimu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (MOEST).

Wakati ma-AEK wana maoni chanya juu ya mambo mengi ya majukumu yao, hawaridhiki sana na fursa za kupanda vyeo/daraja, mishahara, na tuzo pamoja na kuwa wanakabiliwa na kushughulikia mahitaji kutoka kwa watendaji mbalimbalii ndani ya mfumo.

Jacobus Cilliers ni profesa msaidizi katika Shule ya Sera ya Umma ya McCort ya Georgetown na sehemu yaTimu ya Utafiti ya RISE nchini Tanzania. Kabla ya kujiunga na McCourt alifanya kazi katika Mfuko wa Tathmini yaAthari za Kimkakati katika Benki ya Dunia na pia alikuwa mshiriki mwenza wa masomo ya baada ya udaktari wa filosofia katika Skuli ya Serikali ya Blavatnik, Oxford. Utafiti wake umejikita katika eneo la kutumia uchumi wa mtu mmoja mmoja kwa maendeleo, kwa kuzingatia utoaji wa huduma za msingi za elimu. Miradi ya sasa ya utafiti ipo nchini Kenya, Afrika Kusini, na Tanzania. Amechapicha majarida bora kama vile Sayansi, Jarida la Uchumi wa Umma. Na Jarida la Rasilimali watu.

Shardul Oza ni Meneja Mwandamizi wa Programu ya Timu ya Utafiti ya RISE nchini Tanzania akitokea Washington DC. Akifanyia kazi Georgetown's Initiative on Innovation, Development and Evaluation (gui2de), anahusikana usimamizi wa jumla utekelezaji na wa mradi wa RISE Tanzania.Shardul ana uzoefu na tafiti za tathmini za kimatokeo, akiwa amefanya kazi katika mashirika kadhaa yaliyo mstari wa mbele katika 'harakati za sera za kiushahidi' kote Asia Kusini, Africa Mashariki na Marekani

Citation:

Cilliers, J. and Oza, S. 2020. The Motivations, Constraints, and Behaviour of Tanzania's Frontline Education Providers. 2020/023. https://doi.org/10.35489/BSG-RISE-RI_2020/023

RISE is funded by: UKaid from the British people; Australian Aid; Bill & Melinda Gates foundation